**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

Simu/Nukushi Na **026-2502360**
Barua pepe: singidarrh@afya.go.tz
Tovuti:www.singidarrh.go.tz

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,
Mkoa wa Singida,
S. L. P. 104,
**SINGIDA.**

Unapojibu tafadhali taja:
**Kumb.Na.MB.329/377/01/11**

**22.05.2025**

Wananchi wote,
**TANZANIA**

**YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA KUJITOLEA**

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida anawatangazia wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi za kazi za kujitolea. Nafasi husika ni kama ifuatavyo:-

**1.0 AFISA MUUGUZI MSAIDIZI DARAJA LA II - NAFASI 8**

**2.0 Sifa za mwombaji**

i. Awe Stashahada (Diploma) ya Uuguzi, kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania.
ii. Awe na ujuzi/uzoefu wa taaluma ya Uuguzi.
iii. Awe raia wa Tanzania na ambaye hajawai kushtakiwa kwa makosa ya jinai

**2.1 Majukumu yake:**

i. Kutoa huduma za uuguzi.
ii. Kukusanya takwimu muhimu za afya.
iii. Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake.
iv. Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya.
v. Kutoa huduma za kinga na uzazi.
vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**3.0 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI:**

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45;
2. Kila mwombaji anatakiwa aambatishe nakala ya vyeti vya elimu ya sekondari na taaluma vinavyohitajika kulingana na kada husika kama ilivyofafanuliwa katika tangazo hili;

3. Kila mwombaji aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa;
4. Uwasilishaji wa vyeti vya kugushi utapelekea kuchukuliwa hatua za kisheria**;**
5. Mwombaji aambatanishe wasifu binafsi (CV) akionesha uzoefu, namba za simu, anuani yake na anuani za wadhamini watatu (3) wa uhakika.
6. Mwombaji aambatishe picha ndogo (Passport size) mbili (2) kwenye barua ya maombi;
7. Leseni pamoja na vyeti vya usajili kutoka Baraza la Uuguzi na Ukunga.
8. Mwombaji aambatanishe nakala ya kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA**.**
9. Waombaji watakaokidhi vigezo wataitwa kwenye usaili na watakaoshindwa kuzingatia masharti ya tangazo hili hawataitwa;
10. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 05.06.2025 saa 9:30 Alasiri.
11. Maombi yote yatumwe na yawasilishwe **katika ofisi ya masijala ya wazi au barua pepe; barua@singidarrh.go.tz kwa anuani ifuatayo: -**

Mganga Mfawidhi,
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida ,
S.L.P 104,
**SINGIDA.**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA;**

*Dkt: David J. Mwasota,*
**KAIMU MGANGA MFAWIDHI**
**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA**
**SINGIDA.**

MEDICAL OFFICER INCHARGE
SINGIDA REGIONAL REFERRAL HOSPITAL,
P. O. Box 104
SINGIDA